


## MAKAO MAKUU DODOMA

# Tume yapongezwa kuunganisha walimu

Na Sifa Lubasi

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk Charles Msonde amesema kuwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imekuwa kiungo muhimu cha kuwaunganisha walimu na kuleta utulivu.

Alisema hayo jana wakati wa kikao cha baraza la wafanyakazi wa tume hiyo na kuongeza kuwa TSC imekuwa ni kiungo muhimu cha kuwaunganisha walimu hali iliyosaidia kuleta utulivu.

"Ukiona kuna utulivu wa walimu ni kazi nzuri ya tume na serikali inayohakikisha inachukua hatua thabiti," alisema.

Msonde alisema ubora wa elimu umekuwa ukitegemea utulivu wa walimu na utendaji kazi wao, lengo ni kuwa na utendaji wenye kuleta tija.

"Kulikuwa na changamoto za jengo lakini fedha zimeshatolewa na tume imepokea fedha kwa ajili ya kununua magari na vifaa mbalimbali kwa ajili ya ofisi zake," alisema na kuongeza kuwa walimu 54,000 wanatarajiwa kupandishwa madaraja.

"Baada ya uhakiki wa taarifa za walimu imeonesha kuwa walimu wapatao 52,551 wamefuzu vigezo vya kupandishwa madaraja," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Zainabu Katumba alisema serikali imetoa Sh bilioni 1.3 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la utawala na kuitaka Suma JKT iliyopewa jukumu la ujenzi wa jengo hilo, kuongeza kasi ili jengo likamilike kwa wakati.

Alitaka mkutano huo uwe chachu ya kuleta mabadiliko kwa wajumbe kutoa hoja ambazo zitasaidia kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Awali Mwenyekiti wa baraza hilo, Paulina Mkwama alisema, "tunatambua maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhudumia Watanzania na sasa majengo ya tume yanajengwa na watumishi watafanya kazi katika mazingira mazuri".

## Kiwanda cha mvinyo chaleta neema

Na Magnus Mahenge

MJASIRIAMALI Mwanga Chibago amejenga kiwanda cha mvinyo ambacho kimekuwa mkombozi wa wakulima wa zabibu waliokuwa wanakosa soko la zao hilo kwa muda mrefu.

Chibago ambaye amepambana kwa miaka 12 anakuwa mjasiriamali wa kwanza katika Kata ya Mvumi wilayani Chamwino kujenga kiwanda cha mvinyo cha Mkombozi baada ya kuanza jitihada hizo tangu mwaka 2013.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha mvinyo cha Mkombozi, Chibago ambaye ndiye Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho aliwashukuru viongozi wa dini, kisiasa na wananchi wa Mvumi na maeneo ya jirani kwa kumtia moyo kuanzisha kiwanda hicho.

"Kwa namna ya pekee nawashukuru viongozi mbalimbali na wananchi wa kata na tarafa ya Mvumi na Makang'wa kwa kunitia moyo na jitihada zenu, kisingeweza kujengwa na leo kuzinduliwa," alisema.

Chibago pia alilishukuru Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na kusema kuwa watakuwa chini ya Sido kwa miaka saba wakiendelea kukua.

Akizungumzia historia fupi ya uanzishwaji wa kiwanda hicho, Chibago alisema, "tulianza kwa kuandika andiko kwenda kuomba mkopo Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) wa kufanyia kazi mbili, kwanza kuendeleza shamba la zabibu la umwagiliaji na pili kujenga kiwanda… benki hiyo ilisaidia kwa kutoa mkopo wa shilingi milioni 120 tukaendeleza shamba lenye takribani ekari 11".

Kipindi chote hicho walikuwa wakiendesha shamba na ilipofika mwaka 2022, wakaenda Benki ya NMB na kukopa Sh milioni 50 ili kuimarisha kiwanda.

Chibago aliwahimiza wananchi wa Mvumi kupenda kinywaji cha mvinyo kwa sababu wamekuwa wadau wa kweli na kuongeza kuwa soko la kinywaji hicho liwe wao wenyewe kwanza.

Awali Kaimu Meneja wa Sido, Nyangusi Meitalami ambaye alikuwa mgeni rasmi alisema viwanda ni muhimu kwa sababu vinaongeza thamani ya mazao na vinaongeza ajira.

"Kiwanda hiki kimeajiri watu zaidi ya 20, hizo ni ajira ambazo ni za moja kwa moja na kuna ajira ambazo sio za moja kwa moja nyingi sana," alisema.

Meitalami alisema Sido ina jukumu la kuhamasisha viwanda vidogo na kiwanda cha mvinyo cha Mkombozi ni kimojawapo.

Kiwanda hicho kimeanzishwa kwa lengo la kutatua changamoto za wakulima wa zabibu.

Alisema, "kikawe mkombozi kwa wananchi wenye zao la zabibu hasa wa eneo hili kwa kuwahudumia bila kuwabagua na wanaotaka kujifunza kuanzisha viwanda waruhusiwe".

Naye Diwani wa Kata ya Mvumi- Makulu ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Edison Mdonondo aliahidi kuendelea kushirikiana na kiwanda hicho kwa kuutangaza mvinyo wa Mvumi.

Kwa upande wake Ofisa Uendelezaji Biashara kutoka Sido, Crispin Kapinga aliwaomba wananchi wa Mvumi kujitokeza kuanzisha biashara zao na waende ofisi za shirika hilo kusaidiwa namna ya kuendesha.

# Wafanyabiashara sokoni watakiwa kufanya usafi bila kushurutishwa

Na Sifa Lubasi

MKUU wa Kitengo cha Usafi na Udhibiti wa taka ngumu Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro amewataka wafanyabiashara ndani ya masoko kuhakikisha wanaondoa taka kwenye maeneo yao badala ya kusubiri kusimamiwa au kushurutishwa na viongozi.

Alitoa rai hiyo wakati akizungumza na wafanyabiashara wa soko la wazi la machinga baada ya kumalizika kwa usafi. Aliwataka wafanyabiashara kuwajibika wenyewe kuondoa taka kwenye maeneo yao, badala ya kusubiri kushurutishwa na kusimamiwa na viongozi ukizingatia kuwa wao ni wazalishaji wakubwa wa takataka.

"Suala la uondoshaji wa taka siyo jukumu la kusimamiwa na viongozi bali ni la kila mtu, hivyo niwatake wakazi wa jiji kuhakikisha wanafanya usafi wa mazingira bila kusubiri kusimamiwa," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Afya na Usafishaji wa Jiji la Dodoma, John Lugendo aliwataka wafanyabiashara wanaoleta matunda kutoka mikoani wahakikishe vifungashio vinavyotumika vinapelekwa dampo badala ya kuvitupa hovyo na kusababisha uchafuzi wa mazingira kwenye maeneo husika.

Alisema matunda kama matikiti maji, ndizi na nyanya yamekuwa yakiletwa kwenye vifungashio vikiwa vimefunikwa kwa pumba, majani ya migomba na nyasi badala ya kuondoka navyo huachwa na kusababisha kuwa na uchafu sokoni.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Fungo akizungumza na wafanyabiashara hao alisema kumekuwepo na changamoto ya wananchi ya kutupa taka katika mitaro ya maji ya mvua, barabarani, vichaka ambalo limekuwa ni kero kwa watumiaji wa maeneo hayo kutokana na mwonekano wa mandhari usioridhisha.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma itaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo hayo mbalimbali ikiwemo kwenye masoko kwa kipindi chote kikiwemo cha msimu wa mvua ili kuhakikisha usafi wa mazingira unakuwepo wa kudumu kila wakati.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

PDPC

UHURU NA UMOJA

TAARIFA KWA UMMA

WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inapenda kuujulisha Umma kwamba imeanza usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kama ilivyolekezwa katika kifungu Na. 14(1) cha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya Mwaka 2022.

Aidha, Tume imetoa muda wa miezi sita (06) kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi kujisajili kwenye mfumo wa Usajili unaopatikana kupitia tovuti ya Tume, www.pdpc.go.tz

Tume itaendelea kutoa ushauri na msaada wa kitaalam chini ya dawati la huduma kwa wateja kupitia namba za simu 0718462536, 0736110505, 0744057652, 0615779070 au kupitia baruapepe helpdesk@pdpc.go.tz

Emmanuel L. Mkilia
Mkurugenzi Mkuu

www.pdpc.go.tz Tume ya Ulinzi wa Tarifa Binafsi